**NAFASI YA KAZI – NAHODHA WA MASHUA**

Six Rivers Africa (SRA) ni shirika lisilo la kiserikali (NGO) linalojihusisha na uhifadhi wa wanyamapori na mazingira kwa lengo la kulinda, kurejesha na kuhifadhi ubora wa maeneo ya hifadhi, pamoja na kuongeza idadi ya wanyamapori ili vizazi vijavyo viweze kufurahia maliasili hizi. Shirika linatekeleza mradi wa ufugaji nyuki kwenye pori la akiba la ILUMA, pembezoni mwa mto Kilombero, na hivyo anahitajika dereva wa mashua kwa ajili ya kutekeleza kazi za mradi huo.

**Kazi:** Nahodha wa Mashua

**Eneo la kazi:** Ifakara – Morogoro

**Anaripoti kwa:** Afisa Mradi wa Ufugaji Nyuki

**Maelezo ya Kazi**

Nahodha wa mashua atakuwa na jukumu la kusafirisha kwa usalama maafisa mradi, wafugaji nyuki, vifaa na mahitaji yote ya kazi wakati wa shughuli za kufuatilia mizinga na uhamasishaji. Ataakikisha usalama wa abiria na mizigo, kufanya matengenezo madogo ya mashua na injini, na kufuata kanuni zote za usalama na masharti ya uendeshaji mashua.

**Majukumu Makuu**

- Kuhakikisha anafika kwa wakati na kuwa tayari kwa safari zote zilizopangwa.
- Kuendesha mashua kwa usalama na kufuata sheria na kanuni za usafiri majini za Tanzania.
- Kuhakikisha usalama wa abiria na mizigo (ikiwemo vifaa vya ufugaji nyuki) wakati wa safari.
- Kufanya ukaguzi wa usalama na matengenezo madogo kabla na baada ya kila safari.
- Kutunza usafi na hali nzuri ya mashua.
- Kuripoti mara moja (ndani ya saa 3) matatizo au hitilafu za mashua kwa msimamizi.
- Kutunza kumbukumbu sahihi za safari, matumizi ya mafuta, na matengenezo kwenye vitabu vilivyotolewa.
- Kuhakikisha mashua na ijini yake vinahifadhiwa sehemu salama wakati inapokuwa haitumiki.
- Kuendesha mashua kwa uangalifu bila kasi au uendeshaji holela.
- Kupendekeza na kufuata tahadhari za usalama kwa abiria na vifaa wakati wa kazi.

**Sifa za Muombaji**

- Awe na leseni halali ya uendeshaji mashua inayotambulika na Mamlaka ya Usafiri Majini Tanzania (TMA).
- Awe na uzoefu wa kuendesha mashua katika mito (Mwenye uzoefu na Mto Kilombero atapewa kipaumbele).
- Uwezo wa kufanya matengenezo madogo ya mashua.
- Awe na umakini mkubwa wa usalama na uwezo mzuri wa kuwasiliana na watu.
- Uzoefu au uelewa wa kazi za uhifadhi wa mazingira, wanyamapori au miradi inayohusiana.
- Uelewa wa tabia za wanyamapori na tahadhari za usalama hasa katika maeneo yenye wanyama hatarishi kama viboko na mamba.
- Awe ana uwezo mzuri wa kuogelea, hasa katika maji yenye kina kirefu.

Barua ya maombi, wasifu (CV) zitumwe kupitia barua pepe: info@sixriversafrica.com. Mwisho wa kutuma maombi: **4 Novemba 2025**